

bara ya Sengerema - Nyehunge (km 54.4) kwa kiwango cha lami na Mwakilishi kutoka kampuni ya...
gharama takribani Bilioni 73 Mkoani Mwanza. Barabara hiyo ni sehemu ya mtandao wa barabara inayounganiisha Mkoa
wa Mwanza na Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma. **PICHA: WIZARA YA UJENZI**

NIPASHE UK 10.

Wanaogomea chanjo ya mifugo waonywa

Na Alex Sayi MASWA

MKUU wa Wilaya ya Maswa, mkoani Simiyu, Aswege Kaminyoge, amewaonya wafugaji wote wanaogomea utoaji wa chanjo kwa mifugo inayoyoendelea katika kata 36 wilayani hapa.

Amesema, chanjo hiyo ni kwa ajili ya kunusuru mifugo yao na magonjwa mbalimbali ili waendeele kufuga kwa tija.

Kaminyoge alitoa onyo hilo katika kata ya Zanzui na kuwataka wafugaji kutohusisha chanjo hiyo na Kampeni lililositishwa

kwa muda na serikali ya kuvisha ng'ombe hereni.

"Wafugaji jitokezeni kuchanja mifugo yenu ili isipatwe na magonjwa na kampeni hii haina uhusiano wowote na uvishaji wa hereni mifugo, hivyo mifugo yote ni lazima ichanjwe," alisema. Pia, aliwataka watendaji wa kata zote kuhakikishe kampeni hiyo inafanyika kwa uwazi kwa kuwashirikisha wafugaji ili kuwapatia taarifa mapema na kuondoa malalamiko ikiwa ni pamoja na maofisa mifugo kutoa vibali kwa wafugaji wataochanja mifugo yao.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Maswa, Onesmo Makota, alisema kampeni hiyo ni takwa la kisheria na imo katika la Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hivyo wafugaji wanapaswa kujitokeza kuchanja mifugo yao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halimashauri hiyo, Daktari wa Mifugo wa Wilaya, James Kawamala, alisema kwa mujibu wa takwimu za mifugo za mwaka 2017, halimashauri ina ng'ombe 305,640, Mbuzi 122,256 na kondoo 76,410.

Kwa sasa, alisema chanjo hiyo

inahusisha magonjwa mawili ambayo ni homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) na sotoka ya mbuzi na kondoo kati ya magonjwa II ya mifugo. Alisema gharama ya chanjo hizo ni Sh. 800 kwa kila ng'ombe na Sh. 400 kwa kila mbuzi na kondoo.

Ng'wandu Ndoleleji, mkazi na mfugaji wilayani hapa, alishukuru kwa kufikishiwa huduma hiyo karibu huku akiahidi kushiriki kikamilifu kutokana na kutokupata huduma hiyo kwa zaidi ya miaka mitatu huku akiomba serikali kupunguza gharama za uchanjaji wa mifugo hiyo.

na utoaji
tia maku
wakulim
hadi mw
mmoja.

Pia alis
nanchi v
bima pin
wamefik
unaomh
pitali ku
kuwa na
kadi wa
bayo si
bima hi
si kwa d
ulinzi w
nanchi

Alisem
eandaa
majang
kutoing
kuwa k
kuuza p
ma za t

Tafiri sasa kutathmini mazingira ya maziwa

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi (Tafiri) imepanga kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira kwa awamu katika maziwa yote nchini.

Tayari katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/23, imeanza kufanya tathmini katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali la Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga (CCM).

Kamonga alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha Ludewa kwa ajili ya miradi ya ufugaji samaki kwenye vizimba ndani ya Ziwa Nyasa.

Ulega alisema ufugaji samaki kwa vizimba ziwani unafanyika katika maeneo yaliyokidhi vigezo

vya kisheria na kitaalamu.

Katika mwaka 2023/24, serikali imepanga kuendelea kufanya tathmini katika Ziwa Nyasa ikiwemo Ludewa ili kutambua maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki katika vizimba.

Pia, serikali itawezesha Tafiri kufanya majaribio ya ufugaji samaki kwa kushirikiana na wananchi utakaojumuishia uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina ya magege na ufugaji wake kwa vizimba.

Alisema hatua hii inalenga kuwajengea uwezo wananchi wa ufugaji samaki pindi tathmini itakapokamilika.

"Vilevile hatua hii itawawezesha wananchi wa Ludewa na Ziwa Nyasa kwa ujumla kunufaika na fursa za mikopo zilizopo kwa ajili ya kuwezesha ufugaji samaki kwa vizimba," alisema.